Bwana Yesu Kristo anakuja tena duniani hivi karibuni. Hii ni ahadi yake aliyofanya wakati bado alikuwa katika dunia hii miaka 2000 iliyopita (Yn 14:1-3). Jinsi gani tunaweza kujua kwa uhakika kuwa Yeye hakika atarudi? Tafadhali soma unabii (utabiri) ambao Bwana Yesu Mwenyewe alisema kuwa utafanyika katika nyakati za mwisho. Ukisoma kwa makini maandiko haya na kulinganisha na matukio ambayo yanayotokea katika dunia sasa inathibitisha kwamba Bwana Yesu kweli atakuja katika muda wa maisha yetu.

## 1 KUHARIBIWA KWA HEKALU

Alipokuwa akitoka nje ya Hekalu, mmojawapo wa wanafunzi wake akamwambia, "Mwalimu, ona jinsi mawe haya na majengo haya yalivyo maridadi!" Yesu akamjibu, "Unayaona majengo haya yalivyo makubwa? Hakuna hata jiwe moja litakalobaki juu ya jingine, yote yatabomolewa (Mathayo 24:1-2, Mk 13:1-2, Lk 21:5-6).

## 2 ISHARA ZA KUJA

Alipokuwa ameketi kwenye mlima wa Mizeituni akiliangalia Hekalu, Petro, Yakobo, Yohana na Andrea, walikuja kwake na walimwuliza faraghani, "Tafadhali tuambie, mambo haya yatatokea lini? Na ni ishara gani zitaonyesha kuwa karibu yatatimia?" (Matt 24:3, Mk 13:3-4; Lk 21:07).

## 3 WADANGANYIFU WATATOKEA

Yesu akajibu akawambia, "Jihadharini msije mkadanganywa. Maana wengi watakuja wakitumia jina langu, na kusema, 'Mimi ndiye Kristo' na 'Wakati umekaribia' nao watawapotosha wengi. Msiwafuate (Mathayo 24:4-5, Mk 13:5-6, Lk 21:08).

## 4 VITA NA TETESI ZA VITA

Wakati mkisikia habari za vita, misukosuko, na tetesi za vita, msitishike- msiwe na hofu; kwa maana haya hayana budi kutokea; lakini mwisho utakuwa bado (Matt 24:6, Mk 13:07, Lk 21:09).

## 5 VITA VYA KIKABILA | MATETEMEKO|NJAA|MAGONJW

AKisha akawaambia: "Taifa moja litapigana na taifa lin gine na utawala mmoja utapigana na utawala mwingine. Kutaku wepo na matetemeko ya ardhi, njaa kali na magonjwa ya kuambukiza katika sehemu mbalimbali; kutakuwa na matukio ya kutisha na ishara kuu kutoka mbinguni (Mathayo 24:7, Mk 13:08, Lk 21:10-11).

## 6

Yote haya ni mwanzo wa uchungu (Matt 24:8, Mk 13:08).

## 7 MATESO KWA WAKRISTO

Lakini ninyi jihadharini. Kwa maana watu watawapeleka mahakamani na mtapigwa mijeledi katika masinagogi. Mutawekwa katika jela, kisha mtasalitiwa, mtateswa na kuuawa. Mtashtakiwa mbele ya watawala na wafalme kwa sababu ya jina langu, ndipo mtapata nafasi ya kutoa ushuhuda (Matt 24:9; Mk 13:09, Lk. 21:12-13).

## 8

Mtakapokamatwa na kupelekwa mahakamani, msiwe na wasiwasi juu ya matayarisho ya utetezi wenu kabla ya mashtaka. Semeni lo lote litakalowajia wakati huo, kwa sababu maneno mtakayosema si yenu bali yatatoka kwa Roho Mtakatifu. Kwa maana nitawapa maneno na hekima ambayo maadui zenu hawataweza kukataa au kupinga (Mk 13:11; Lk 21: 14-15).

## 9 USALITI KATIKA FAMILIA

Halafu wengi watakwazika. Ndugu atamsaliti ndugu yake auawe; baba atamsaliti mwanae, marafiki na ndugu; Watoto watawaasi wazazi wao na kusababisha wauawe. Kila mtu atawachukia kwa sababu ya jina langu; Lakini hautapotea hata unywele mmoja wa vichwa vyenu! Simameni imara nanyi mtaokoa nafsi zenu (Mathayo 24:9-10, Mk 13:12-13, Lk 21:16-19).

## 10 UPENDO UTAPOA

Kwa sababu uovu utakuwa umeenea sana, upendo wa watu wengi utapoa. Lakini mtu atakayesimama imara mpaka mwisho, ataokolewa (Mathayo 24:12-13).

## 11

Na hii **INJILI YA UFALME** itahubiriwa ulimwenguni pote, kama ushuhuda kwa mataifa yote. Ndipo mwisho utafika (Mathayo 24:14, Mk 13:10).

## 12 CHUKIZO LA UHARIBIIFU YERUSALEM

Mkiona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, fahamuni kwamba karibu utaangamizwa (Lk 2 1: 2 0). Mtakapoona lile chukizo la uharibifu linalozungumzwa na nabii Danieli limesimama mahali Patakatifu - msomaji na aelewe - basi wale walioko Yudea wakimbilie milimani. Aliyeko juu ya nyumba asishuke kuchukua vitu vyake ndani. Aliyeko shambani asirudi nyumbani kuchukua vazi lake (Mathayo 24:15-18;Mk 13:14-16, Lk 17:31; 21:21). Ole wao wanawake watakaokuwa na mimba na watakaokuwa wakinyonyesha siku hizo! Ombeni ili mtakapokuwa mnakimbia, isiwe ni kipindi cha baridi au siku ya sabato (Matt 24:19-20, Mk 13:17-18, Lk 21:23). Wengine watauawa kwa silaha na wengine watachukuliwa mateka na kupelekwa nchi mbalimbali. Na Yerusalemu itamilikiwa na watu wa mataifa mengine mpaka muda wa mataifa hayo utakapokwisha (Lk 21:24).

## 13 WAKATI WA TAABU YA YAKOBO

(Jer 30:6-7)

Kwa maana kutakuwa na dhiki kuu ambayo haijawahi kutokea tangu mwanzo wa dunia mpaka sasa na ambayo haitatokea tena. Kama siku hizo zisingepunguzwa, hakuna hata mtu mmoja ambaye angesalimika, lakini kwa ajili ya wale walioteuliwa na Mungu, siku hizo zitapunguzwa (Mathayo 24:21-22; Mk 13:19-20, Lk 21:23). Kwa sababu huu utakuwa wakati wa kulipiza kisasi ili yale yote yaliyosemwa kwenye Maandiko yatimie (Lk 21:22).

## 14 KRISTO WA UONGO NA MANABII

Wakati huo mtu akiwaambia, 'Tazama! Kristo yuko hapa!' au 'Kristo yule pale!' msisadiki. Kwa maana watatokea Kristo na manabii wa uongo na watafanya ishara za ajabu na miujiza mingi ili kuwadanganya, hata ikiwezekana, wateule wa Mungu. Kwa hiyo jihadharini kwa maana nimewaambia mambo haya kabla hayajatokea (Mathayo 24:23-24, Mk 13:21-23). Kwa hiyo wakiwaambia, 'Yule kule nyikani,' msitoke. Au wakisema, 'Yuko chumbani' msiamini. Kwa maana kama vile umeme unavyomulika mbingu kutoka upande mmoja wa mashariki na kuangaza upande mwingine wa magharibi, ndivyo itakavyokuwa kuja kwangu mimi Mwana wa Adamu (Matt 24:26-27, Lk 17:23-24).

## 15 ISHARA KATIKA MBINGU

Mara baada ya dhiki ya wakati huo, jua litatiwa giza, mwezi hautatoa mwanga wake tena, na nyota zitaanguka kutoka mbinguni; nguvu za anga zitatikisika (Mathayo 24: 29; Mk 13:24-25, Lk 21:25). Kutakuwa na matukio ya ajabu



kwenye jua, mwezi na nyota. Hapa ulimwenguni, mataifa yatakuwa katika dhiki na wasi wasi kutokana na ngurumo na dhoruba za kutisha zitakazotokea baharini. Watu watakufa moyo kwa hofu na wasiwasi kuhusu yale wanayoogopa kuwa yataukumba ulimwengu (Lk 21:25-26).

16 Ndipo **ISHARA YA MWANA WA ADAMU** itaonekana angani na watu wote ulimwenguni wataomboleza. Nao watamuona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya angani, katika uwezo na utukufu mkuu. Na atawatuma malaika wake kwa sauti kuu ya tarumbeta na watawakusanya wateule wake kutoka pande zote nne za dunia, kutoka mwisho mmoja wa dunia hadi mwisho wa mbingu (Mathayo 24:30-31; Mk 13:26-27, Lk 21:27).

17 Mambo haya yakianza kutokea, simameni imara, mjipe moyo, kwa kuwa ukombozi wenu unakaribia (Lk 21:28).

18 Akawaambia mfano, "Utazameni mtini na miti mingine yote. Inapochipua majani, mnatambua ya kuwa wakati wa mavuno uko karibu. Hali kadhalika, mkiyaona mambo haya yanatokea, fahamuni kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia (Matt 24:32-33, Mk 13:28-29, Lk 21:29-31). Hakuna ajuaye siku wala saa, hata malaika mbinguni wala Mwana, isipokuwa Baba peke yake (Mathayo 24:36, Mk 13:32).

19 Kama ilivyokuwa **WAKATI WA NUHU**, ndivyo itakavyokuwa atakaporudi Mwana wa Adamu. Kwa maana siku zile kabla ya gharika, watu walikuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa, mpaka siku ile Nuhu alipoingia kwenye safina. Nao hawakujua ni nini kitatokea mpaka gharika ilipokuja ikawakumba wote. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kuja kwa Mwana wa Adamu (Matt 24:37-39, Lk 17:26-27).

20 Kama zilivyokuwa **NYAKATI ZA LUTU**: Watu walikuwa wakila, wakinywa, wakifanya biashara, wakilima na kujenga. Lakini siku ile Lutu alipoondoka Sodoma, moto ulishuka kutoka mbinguni ukawaangamiza wote. Ndivyo itakavyokuwa siku ambapo Mwana wa Adamu atakapotokea kwa utukufu (Lk 17:28-30).

21 Kumbukeni yaliyompata mke wa Lutu. Mtu yeyote anayejaribu kusalimisha maisha yake atayapoteza; na yeyote atakayekuwa tayari kuyapoteza maisha yake atayaokoa (Lk 17:32-33).

22 Nawaambia, usiku huo watu wawili watakuwa wamelala kitanda kimoja; mmoja atachukuliwa, mwingine ataachwa. Wanawake wawili watakuwa wanatwanga pamoja; mmoja atachukuliwa na mwingine ataachwa. Wanaume wawili watakuwa wanafanya kazi pamoja shambani; mmoja atachukuliwa na mwingine ataachwa (Mathayo 24:40-41; Lk 17:34-36). Wakamwuliza, "Haya yatatokea wapi Bwana?" Akawaambia, "Pale ulipo mzoga, ndipo tai wanapokutanika (Mathayo 24:28, Lk 17:37).

23 **KESHENI NA KUOMBA**
Ni kama mtu anayesafiri na kuwaachia watumishi wake madaraka, kila mtu na wajibu wake; kisha akamwambia mlinzi wa mlango awe macho. Kesheni basi, kwa sababu hamjui ni lini bwana mwenye nyumba atarudi. Anaweza akaja jioni, au usiku wa manane au alfajiri au mapambazuko. Kama akija ghafla, pasipo ninyi kumtazamia, asije awakute mmelala (Mk 13:34-36).

24 Lakini fahamuni kwamba, kama mwenye nyumba angalifahamu ni saa ngapi za usiku ambapo mwizi atakuja, angalikaa macho asiache nyumba yake ivunjwe. Kwa hiyo ninyi pia lazima muwe tayari kwa maana Mwana wa Adamu atakuja saa msiyo nitegemea (Mathayo 24:43-44).

25 Jihadharini msije mkatawaliwa na ulafi, ulevi na wasiwasi wa maisha haya, kisha siku ikafika pasipo ninyi kutazamia. Kesheni na kuomba, kwa maana hamjui wakati mambo haya yatakapotokea. Kwa kuwa siku hiyo itawakumba watu wote waishio duniani (Mk 13:33, Lk 21:34-35).

26 Na ninayowambia nyinyi, nawambia wote: kesheni na kuomba ili Mungu awawezeshe kuepuka yale yote yatakayotokea na muweze kusimama mbele ya Mwana wa Adamu (Lk 21:36).

27 Nawaambieni kweli, hakika kizazi hiki hakitapita kabla mambo haya hayajatokea. Mbingu na dunia zitatoweka, lakini maneno yangu hayatapita kamwe (Matt 24:34-35, Mk 13:30-31, Lk 21:32-33).


**Mcheni Mungu na kumtu kuza kwa maana saa ya kutoa hukumu yake imefika; Mwabuduni yeye aliyeumba mbingu, dunia, bahari na chemchemi za maji (Ufunuo 14:7).**

**MUDA WA KUSUBRI ZAIDI UMEKWISHA!**

Ufalme wa mbinguni umekaribia sasa. Tubuni na kuiamini Injili.

**Hakika, Bwana Yesu Kristo anakuja tena haraka. Je, uko tayari kukutana na Bwana Mungu wako?**

Kwa habari zaidi angalia Angel TV
www.angeltv.org | www.jesusministries.org




# Injili Ya Ufalme

KISWAHILI | SWAHILI